**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**Episode 07**

**Title: With Passion to Success: the Kenyan photographer Charles Adede**

**Author: Eric Ponda**

**Editors: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

## Characters (O-Töne, Clips) / Narrators

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | x | | Unimportant | |
| Narrator | | x | Unimportant | |
| Charles Adede (clip) | | x | 37 | English |
| Pilli Mwakio (clip) | x | | 25 | English |

**Intro:** Hujambo na kwa mara nyingine karibu kwa makala ya saba kwenye mfululizo huu wa vipindi vya "Learning By Ear", "Noa Bongo Jenga Maisha yako" tukiwaangazia Wajasirimali chipukizi waliofaulu Barani Afrika na wanao wajibika kuboresha maisha miongoni mwa jamii wanamoishi.

Katika makala ya leo tunafunga safari hadi mji mkuu wa Nairobi nchini Kenya ambako tunakutana na mpiga picha ambaye ameachilia ngazi taaluma ya uana sheria na kugeukia shughuli za upigaji picha.

1. **SFX: (At the studio Shutter Speed Nairobi, steel gates open)**

2. **Narration:**

   Nje ya lango linaloelekea ofisini mwake, bado limekitwa bangp kubwa lenye maandishi "Legal Resource Foundation". Ukumbusho wa shughuli za kisheria zilizokuwa zikiendelea katika ofisi hizi.

   Ni Ijumaa mwendo wa saa moja na nusu hivi asubuhi, lakini tayari wateja wameanza kumiminika katika ofisi yake, kuweka miadi ya kazi zao mwishoni mwa wiki. Lakini si kutafuta ushauri wa kisheria au kwenda safari ya likizo. Wanatafuta miadi na Mpiga picha huyu chipukizi. Akiwa ameketi ofisini mwake iliyoko mtaa wa watu wenye maisha ya kadri jijini Nairobi, tayari Shajara ya Charles Adede imejaa..

3. **SFX: conversation with customer on mobile phone**

**Narration**

Huku akiwa mwenye kutabasamu kila wakati, mwanasheria huyu ambaye ameiasi taaluma yake ya Uanasheria na kuingilia shughuli ya upigaji picha , ananikaribisha ofisini mwake, mkononi tayari akiwa amebeba kamera aina ya Nikon D-90. Lakini kwanza hatuwezi kuendelea na mazungumza yetu hadi atakapokamaliza kuzungumza na simu yake na mkononi, wateja wanaompigia simu mmoja baada ye mwengine.

Tuko katika studio za Shutterspeed, ambazo zimepindukia kuwa maarufu sana nchini Kenyan kutokana na ubora wa picha zake. Na Charles Adede ndie mkurugenzi wa kampuni na mpigaji picha mashuhuri katia kampuni hii.

### 4. Charles Adede (Eng)

"Nilipokuwa mdogo kuna mambo mawili nilitaka kufanya maishani. Nilipenda sana kuwa mwandishi wa habari au mwanasheria. Nilifanikiwa kuwa mwanasheria, na nikapata mafubnzo ya uanasheria, kisha baadaye niakaajiriwa katika kampuni moja ya bima jijini Nairobi, kama mshauri wa masuala ya kisheria kwa kampuni mbali mbali za kutoa huduma za bima… Lakini pia nilitamani sana kuwa mwandishi wa habari au msanii. Sukupata mafunzi ya ya kuwa msanii kama nilivyotaman! Sikupata nafasi hiyo kabisa kwani sikubahatika kujiunga na chuo cha usanii. Lakini sikufa moyo, na fursa nyingine ilikuwa hii upigaji picha. Kwa hivyo nikaamua kujitosa katika sekta hii ya upigaji picha."

### 5. Narration

Upigaji picha ni usanii, na kama ilivyo desturi, katika usanii wa aina yoyote ile, ubora wa sanaa ndio msingi wa ufanisi katika sekta hii, na ni lazima Mtu ajitume kikamilifu.Ujumbe wa picha hutegemea ubora wake. Picha ni chombo cha mawasiliano na ujumbe wake ni mzito kama ilivyo matumizi yake ni mengi, kwani picha mara nyingi huelezea mengi kushinda aina nyingi yoyote ile mawasiliano! Hata hivyo si vijana wengi wanaoweza kuacha taaluma muhimu kama ya Uanasheria na kuingilia kazi ya upigaji picha jinsi alivyofanya Charles Addede.

**6. Charles Adede (Eng)**

"Kwanza ni Uchu. Uchu ni kama mnyama wa ajabu. Wakati nilipokuwa nikifanya kazi kama mwanasheria, nilianza kuwa na uchu wa kuwa mpigaji picha, na uchu huo ulizidi kuongezeka hadi kufika kiwango cha kuanza kupiga picha japo si kwa ustadi vile, yaani mpiga picha chipikizi! Hata hivyo watu walikuwa watazama picha zangu na kuniambia, hheeee. Wewe unaweza kuwa mpigaji picha mashuhuri sana, na unafahamu kwamba kazi hii inaweza kukuletea mapato maishani. Basi sifa hizi zikaanza kunitawala. Nilipindukia kuipenda sana kazi hii, hasa picha zangu nilizopiga, kufikia kiwango cha kuanzisha biashara ndogo mbadala ya shughuli zangu za kawaida kama mwanasheria. Lakini kazi hii ilianza kuimarika na nikaipenda sana mpaka ikafika wakati, wa kuchagua kazi ninayotaka kuendelea nayo baina ya Uanasheria au kuwa mpigaji picha. Hivyo nikaamua kuacha kazi ya uanasheria na kujitosa katika sekta hii ya upigaji picha, ili nione itanifikisha wapi maishani."

**7. Narration:**

September mwaka 2006 ndipo Charles Adede alianza kupiga picha za harusi wakati wa usiku na mwishoni mwa wiki. Lakini anasema haikuwa rasihi!

8. **Charles Adede (Eng)**

"Nialianza kupiga picha katika sherehe za harusi za marafiki zangu wakati wa usiku, ndivyo nilivyoanza kazi hii. Nilitegemea pesa nilizoweka akiba wakati nikifanya kazi. Wakati huo nilikuwa bado sijaoa na maisha yangu yalikuwa ya kawaida tu ya ukapera. Nakumbuka nilikuwa nikitumia kamera ndogo sana aina ya Fuji.. …..japo ilikuwa ndogo lakini ilikuwa nzuri sana…Pia nilitamani sana kupiga picha za video ambayo ni miongoni kwa shughuli tunazofanya katika studio hizi zetu hapa ShutterSpeed."

9. **Narration:**

Kwa mtaji wa kima cha Euro 2000, Charles Adede aliweza kufungua Studio yake. Alinunua vifaa vya studio kama vile Komputa, Kamera ndogo na nyingine ya Video. Lakini uchu wa Charles Adede sasa umemwezesha kupanua biashara yake kufika upeo mkubwa,na kubuni nafasi za kazi kwa vijana wengi sana licha ya kwamba hakuisomea kazi hii.

10. **Charles Adede (Eng)**

"Sasa biashara hii imepanuka sana!, *(laughs….)* hapa tuko na studio za kupiga picha na tunauwezo wa kushughulikia sherere tatu kwa siku, kumaanisha tuna makundi matatu ya wafanyi kazi 4 kila moja, jumla ni wafanyi kazi 12 wanaofanya kazi katika sherehe tatu kwa siku. Kisha tuna studio zetu hapa na tuna kazi nyingi sana. Ama kwa hakika sekta hii linazidi kupanuka. Mara nyingi ukiwa na uchu, na ukijitolea kufanikisha azma yako, bila shaka utaweza kufanya mambo ambayo wengi wasio na azma wanashindwa kufanya hata kama Mtu ameisomea kazi yenyewe, huku yule ambaye hajaisomea akafanya vyema zaidi kwasababu ya kujituma na kuwa na mwelekeo."

**11. SFX, Charles giving instructions, background music, click of a camera.**

**12. Narration**

Studio za Shutterspoeed sasa zina shughuli nyingi. Wateja wanaokuja kuchukua picha au kanda za video zao, huku wengine wakiweka miadi ya kupigwa picha wakati wa sherehe zao. Ndani ya studio zilizojengwa kwa ustadi na kisasa kabisa, tunakutana na mteja mmoja Pili Mwakio, mwanafunzi wa chuo kikuu akijiandaa kupigwa picha. Na Charles Adede ndie mwenye kumpiga picha hizo.

**13. Pilli Mwakio (Eng)**

"Mimi huja katika studio hizi kila mara ninapohitaji kupigwa picha. Ni Studio nzuri sana, mazingira yake ni mazuri na pia wapigaji picha wenyewe ni watu walio na ujuzi. Yaani unauhakika ya kuhudumiwa na watu wanaoifahamu vyema kazi yao! Hebu tazama, fremu za picha, zilivyotengenezwa kwa ustadi, Si zinapendeza sivyo? Picha ni ukumbusho na lazima uhifadhi kumbukumbu zako kwa njia bora zaidi unavyoweza ."

**14. Narration:**

Kama mwanafunzi wa chuo kikuu Pili na wateja wengine wengi wanaimani na huduma nzuri zinazotolewa katika studio hizi za Shutterspeed. Hii ndio imani inayomjenga Charles Adede kufanikisha biashara yake.Mwanzoni ukosefu wa misaada, hasa ya kifedha na ushindani kwenye soko, lilikuwa tatizo kubwa kwa Charles Adede katka kuanzisha biashara hii. Hali inayowatatiza wajasiri mali chipukizi katika mataifa mengi Barani Afrika.Na tatizo hili lilimfanya Charles nusra afilisike na kufunga biashara aliyeipenda kwa moyo wake wote.

**15. Charles Adede (Eng)**

"Ilifika wakati nusra tufunge biashara hii kutokana na ukosefu wa fedha, na biashara hii inayohitaji mtaji mkubwa.Hivyo nililazimika kuuza sehemu ya hisa zangu kununua vifaa na kuwaajiri wafanyi kazi zaidi. Tatizo ni kwamba hakuna taasisi ya kutoa mafunzo kwa wafanyi biashara wadogo wadogo hapa nchini mfano mbinu za usimamizi wa biashara. Na ndio sababu wafanyi biashara wengi hufilisika haraka maana hawana ujuzi wa kusimamia vyema biashara zao.Biashara nyingi zinaendeshwa jua kali, yaani hali ya kubahatisha tu. Tungekuwa na taasisi nyingi za kutoa mafunzo ya biashara, basi tungesema kweli tunapata mafunzo ya kuweza kusimamia vyema biashara. Na hapo tungeweza kubuni nafasi nyingi zaidi za kazi badala ya kusuburi au kuhangaika huku na kule kutafuta kazi za kuajiriwa!"

**16. Narration:**

Hata hivyo lakini Charles hakufika kiwango hicho cha kuendesha biashara yake kijua kali, yaani hali ya kubahatisha. Amekuwa na mipango na utaratibu mzuri wa kusimamia biashara hiyo. Hii ndio sababu Charles sasa anafurahia ufanisi wake. Baada ya kuhangaika kwa muda mrefu soko sasa limefunguka na ana kila sababu ya kutabasamu, anasema!

**17. Charles Adede (Eng)**

Watu wanakiu cha kupata huduma bora. Tatizo kubwa ni kwamba wafanyibiashara wanashindwa kutoa hudumza bora kukata kiu hiki.Wanashindwa kuwapa Wakenya huduma bora wanazohitaji. Kile wakenya wanachohitaji ni huduma bora tu na wako tayari kugharamia huduma hizi, lakini pia ni lazima uonyeshe tajiriba ya hali ya juu katika kazi unayofanya na pia kujitolea katika kila jambo unalofanya!

**18. Narration:**

Kama mwanasheria na sasa mtu anayesimamia biashara yake, Charles Adede anasema kuwa nidhamu ya kazi ndio msingi na changamoto kubwa kwa wajasirimali wengi barani Afrika. Biashara inahitaji Mtu kujitolea na kuwa na mipangilio thabiti ya usimamizi wakati wote. Tatizo kubwa la wafanyibiashara wengi chipukizi ni ukosefu wa mipangilio hali inayochangia pakubwa ongezeko la tatizo la ajira katika mataifa mengi barani Afrika anasema Charles.

19. **Charles Adede (Eng)**

"Vijana wengi hutumia pesa nyingi ambazo si zao kujistarehesha…*laughs)*! Usitumie pesa za mteja kununulia rafiki zako Pombe! Mfano mteja akikupa pesa tuseme euro 500 ili umfanyie, na utumie pesa hizo kwa starehe au kuwanunulia marafiki wako bia utakwama. Wakati ukifika wa kutekeleza kazi hiyo utakuta huna pesa za kutekeleza kazi yenyewe. Kwa hivyo lazima uwe na nidhamu ya hali ya juu katika usimamizi wa pesa. Huo ndio ushauri naweza kuwapa vijana wanaotaka kuanzisha biashara."

**20. Narration**

Charles Adede amekuwa mfano bora wa kuigwa kutoka na uchu wake uliomwezesha kuanzisha biashara yake na sasa anatoa mchango mkubwa kwa jamii kupitia ajira kwa vijana. Juhudi zake za kujitolea kuona anafaulu, zimetoa mwangaza na kuwapa motisha vijana wengi wanaotaka kuiga mfano wake. Na mipango yake ya siku za usoni ni kujenga chuo cha kutoa mafunzo ya upigaj picha kwa vijana wengi wasio na ajira

**Charles Adede (Eng)**

Ukimuona kijana akihangaika na kuomba omba barabarani umpatie shilingi elfu tano sawa na Euro 50, kisha usimwambie jinsi ya kutumia pesa hizo, bila shaka ataenda kununia mavazi au pengine kunywa pombe na atarudi tena pale barabarani kuomba. Suluhisho ni kubuni mazingira bora na kuwapa uwezo vijana wa kuanzisha biashara zao hata kama ni biashara ndogo ndogo**.**

**Outro:**

Tunakushukuru sana, Charles Adede, kwa umaizi huo kuhusu studio zako Jijini Nairobi. Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi hiki cha leo cha “Learning by Ear” Noa bongo jenga maisha yako kuhusu wajasirimali chipukizi wanaotoa mchango wao kwa jamii. Mwandishi wetu ni Eric Ponda, na tunakushukuru pia msikilizaji wa muda wako. Endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au vingine vya Noa Bongo, tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbes. Hadi wakati mwengine tutakapo ungana nasi tena kwa makala nyingine ya Noa Bongo, kwaheri kwa sasa.